

Huduma za Ufikiaji wa Lugha

Huduma za Ufikiaji wa Lugha huhakikisha kuwa wenyewe umilisi mdogo wa kiingereza (LEP) wana ufikiaji sawa, ikiwa ni pamoja na ukalimani wa simu, ukalimani binafsi, tafsiri ya nyaraka muhimu, na mafunzo kwa wafanyakazi wa jiji.

Jiji la Bowling Green hutoa huduma ya ufikiaji wa lugha kwa watu ambao hawazungumzi, kusoma, kuandika au kuilewa lugha ya Kiingereza. Unaweza kupata huduma za ukalimani bila malipo unapohitaji usaidizi au habari kwenye Idara fulani ya Jiji.



Mpango wa 'Jirani Mpya'

Mpango wa 'Jirani Mpya' ni kikao cha kielimu kwa Wafanyakazi wa Jiji na Jamii kujifunza kuhusu historia, mila na tamaduni, vyakula, ngoma na mengineyo kutoka kwenye makundi maalum ya kitamaduni yaliyowakilishwa jijini Bowling Green. Mpango wa 'Jirani Mpya' unafanyika mara moja kwa mwaka.

Uongozi na Mawasiliano

Kuwashirikisha viongozi wa karibu na wakazi anuwai kushiriki mawasiliano mazuri, na kuendeleza mipango, taratibu na jamii kuwa ya kusisimua ambapo vipaji ya kila mtu vinathaminiwa na kukuzwa.

Ufikiaji Sawa

Kupunguza vikwazo vya huduma na ushiriki ili huduma za jiji zipatikane kwa wakazi wote.

Kukuza fursa za ushirikisho wa raia

Kuhakikisha kuwa wageni wanashirikishwa kikamilifu katika maisha ya kiraia, kuungeza ufikiaji wa uongozi, uraia na jamii

Kuza fursa za kiuchumi na elimu

Kuunasa uwezo kamili wa wakazi wote. Wageni wana ujuzi, mali, na elimu, na mifumo ya kuendeleza uchumi i tayari kwa vipaji vipyta na vilivymomo.

Jamii Salama na Inayohusiana

Kukuza uaminifu na kujenga mahusiano kati ya wahamiaji; kuzipokea jamii, kujenga uhusiano ndani na mionganini mwa Idara za Jiji.

Ushirikiano wa Jumuiya za Kimataifa

Ushirikiano wa Jumuiya za Kimataifa wa Jiji la Bowling Green unatumika kuratibu jukumu la Jiji katika kuwasiliana na kufanya kazi kwa ufanisi na jamii anuwai za kimataifa zilizowakilishwa Bowling Green, na kutumika kama mtetezi wa watu wenyewe LEP (Umilisi Mdogo wa Kiingereza) wanaoweza kuwa wanatafuta huduma za Jiji.



Leyda Becker
Mtaalamu wa Huduma za Jamii/
Ushirikiano wa Jumuiya za Kimataifa (270) 393-3766
leyda.becker@bgky.org



Baraza la Ushauri wa Jumuiya za Kimataifa la Mji wa Bowling Green (ICAC)

ICAC huushauri Ushirikiano wa Jumuiya za Kimataifa kuhusu mahitaji ya wakazi wahamiajji na wakimbizi wa Bowling Green. Baraza hiyo hulenga maendeleo ya kiuchumi, ubora wa maisha, usalama wa umma, uchangamshaji wa ujirani na utoaji wa huduma.

Wasiliana nasi:

Leyda Becker
Mtaalamu wa Huduma za Jamii/
Ushirikiano wa Jumuiya za Kimataifa
Huduma za Ujirani na Jamii
707 East Main Avenue
S.L.P 430
Bowling Green, KY
42102 (270) 393-3766
leyda.becker@bgky.org
www.bgky.org/ncs/icl.php

Chuo cha Wamarekani Wapya

Chuo cha Wamarekani ni mpango wa mafunzo ya uongozi unaotolewa bure na kufadhiliwa na Jiji la Bowling Green linalowapa Wamarekani Wapya uwezo wa kuelewa na kushiriki katika Serikali ya Jiji.



Upokezi wa Wamarekani Wapya

Upokezi wa Wamarekani Wapya ni sherehe ya kila mwaka ya kuwatambua wananchi wapya wa Bowlin Green.



Mfumo Mtandao wa Rasilimali wa Amigos

Mfumo Mtandao wa Rasilimali wa Amigos, au Red de Recursos Amigos, ni kundi la mfumo mtandao la viongozi kutoka jamii ya Hispania/Latino katika Bowling Green. Inalenga kuziba pengo la habari kati ya jamii na huduma zilizopo.

Habari-e za Uwiliilugha: Wananchi wanaweza kujijandikisha ili kupokea barua pepe, ikiwemo jarida lilloandikwa kwa lugha mbili (Kihispania na Kiingereza), kwa kutembelea www.bgky.org.

Huduma ya Upokezi wa Jumbe Fupi: Ili kupokea ujumbe mfupi kuhusu habari za Jiji katika Kihispania, tuma ujumbe mfupi "AmigosBG" kwa 555-888

La Nuestra

"La Nuestra" ndicho kipindi cha redio katika lugha ya Kihispania cha pekee jijini Bowling Green, KY. Huuperushwa katika Redio ya WKCT kila Jumapili alasiri kutoka saa 3:00 – 5:00. Ushirikiano wa Jumuiya za Kimataifa huwa wenyeji wa kipindi cha kila wiki kuhusu huduma za Jiji na habari kwa jamii.

